Halmashauri ya
Mji Kasulu

TOLEO NA: 001 | JANUARY 2024

# JARIDA La HALMASHAURI YA MJI KASULU



HABARI KUU

## BILIONI 1.493 ZA BOOST ZAPUNGUZA MSONGAMANO MASHULENI

JAN 29, 2024 | UK 01

Serikali kupitia mradi wa BOOST yajenga madarasa 45 na matundu ya vyoo 68 ambayo yamesaidia kuondoa kero ya mrundikano wa wanafunzi madarasani.

" Kasulu ya Mama Samia tumejitafuta tumejipata hatuna mbambamba "

1



2



3



4



Imetolewa na
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Mji Kasulu.

# 01 BILIONI 1.493 ZA MRADI WA BOOST ZAPUNGUZA MSONGAMANO WA WANAFUNZI MASHULENI.







Wazazi wa Halmashauri ya mji Kasulu waipongeza serikali ya awamu ya sita kupitia kwa Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kupunguza msongamano wa wanafunzi wa shule kufuatia kukamilika kwa mradi wa BOOST ambapo jumla ya bilioni 1.493 zimetumika kujenga vymba 45 vya madarasa na matundu 68 ya vyoo ili kupunguza mrundikano wa wanafunzi mashuleni.

Akizungumza katika moja ya shule mpya ya Murusi iliotokana na mradi huo mara baaada ya usaili wa wanafunzi Janet Ndemeye mzazi wa mwanafunzi amesema, shule hiyo mpya ya Murusi Imeweza kupunguza changamoto ikiwemo wingi wa wanafunzi na kutembea umbali mrefu.

"Napenda kumpongeza Rais Dkt. Samia kwa kutujengea shule hii mpya na nafurahi mjukuu wangu kusomea katika shule hii"

Kwa upande wake mwanafunzi Hadija Juma Hamis amemshukuru Raisi na kusema madarasa mapya yameongeza ari ya kusoma na hivyo kutoa ahadi ya kusoma kwa bidii.

Aidha kwa upande wake Afisa elimu kata ya Murusi Gervas Edward Lugeze Amesema anaipongeza serikali kwa kusimamia ilani ya Chama kwa kuhakikisha miradi iliyopangwa kutekeleza inakamilika.

"Leo nimekuja kukagua shule hii mpya ambayo imegharimu kiasi cha Tsh 361,500,000 ikiwa na vyumba tisa vya madarasa ya shule mpya yenye mkondo mmoja na madarasa mawili ya mfano ya awali.

Mradi huu wa BOOST umelenga kuboresha upatikanaji fursa sawa katika ufunzaji na ujifunzaji bora wa elimu ya awali na msingi Tanzania bara.





# 02 SHANGWE NA FURAHA ZATANDA KWA WANAWAKE WAJASIRIAMALI SOKO LA KUMSENGA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kasulu Ameelekeza mgambo kuacha kuwapiga na kutokuwazuia wakina mama wanaofanya biashara katika makutano ya barabara ya NHC na Msufini iliopo katika kata ya Kumsenga wilayani kasulu.
Ameyasema hayo hapo jana kwenye kikao cha wazi na wafanyabiashara wa soko la kumsenga kilichohusisha Mwenyekiti wa halmashauri, Mkurugenzi mkuu, wakuu wa Idara na vitengo, diwani wa kata ya Kumsenga, ofisi ya kata pamoja na wafanyabiashara wa soko la Kumsenga.
Amesema kuwa ni Marufuku kwa mgambo kuwanyanyasa wakina mama wanaofanya biashara ndogo dogo wakati wa jioni katika eneo hilo.
Aidha Amewataka wafanyabiashara kuwa wasikivu na kufuata sheria na kuacha kuwapiga mgambo.
"Lakini nawaomba na nyinyi mfate utaratibu na mkipangwa msikilize na muacha tabia ya kupiga wagambo".
Pia Mkurugenzi Amelezea kwa kina namna ya kuboresha vibanda vya Halmashauri, akiwataka wafanyabiashara kurekebisha vibanda hivyo wao wenyewe kwa gharama zao na si vinginevyo.
“Wanawadanganya Halmashauri itatengeneza vibanda kwamba mlipe hela kwetu alafu tuwarekebishia sisi hatutapokea hata senti na badala yake mtarekebisha wenyewe kama ni rangi, tofali, simenti mtanunua wenyewe na fundi mtawalipa wenyewe sisi tutaoa mongozo tu ....... Uk 3

cont...Uk 2
mtu akisema mlipe hela huyo ni muongo”
Tumesema vibanda hivi viinuliwe na maboresho yaanzie kwenye renta na kuboresha Muonekano wa Mji vipigwe rangi kwa gharama za mfanyabiashara na wala Halmashauri haina mpango wa kubomoa vibanda hivyo kama inavyosemekana. Ameongeza Mkurugenzi.

Mkurugenzi pia amewataka wafanyabiashara kuingia wenye vibanda kuingia mkataba ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato huku akisisitiza mwisho wa kujaza mikataba hiyo ni Februari 18, 2024 na kua kwa yeyote ambae hatakua na mkataba hatua kali zitachukuliwa juu yake.

## 03 WANANCHI WATAKIWA KUFANYA USAFI KATIKA MAENEO YAO ILI KUEPUKA KIPINDUPINDU



Kufuatiwa baadhi ya maeneo nchini kuripotiwa kuwa na mripuko wa kipindupindu wananchi wa Halmashauri ya Mji Kasulu washauriwa kuchukua tahadhari mapema kwa kufanya usafi wa mazingira yanayoowazunguka ili kuepukana na ugonjwa huo.
Ushauri huo umetolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji kasulu Dollar Rajab Kusenge wakati wa kufanya usafi wa mwisho wa mwezi Jumamosi Januari 27 mwaka huu
Amesisitiza kuwa wananchi pamoja na wafanya biashara wanatakiwa kufanya usafi katika maeneo yao bila yakushuurutishwa na kutunza taka katika vifaa malumu na

“Katika kipindi hiki cha mvua wananchi wakate nyasi kwenye maeneo yao na kwa wafanya biashara kuhifadhi taka katika vitunzia taka kusubiri magari ya taka na pia nitoe rai kwa wale wananchi wanaotupa taka hovyo hasa kwenye mifereji na wale wanaofungulia chemba wakati huu wa mvua waache kufanya hivyo kwani wanaweza kuleta hatari kwa afya zao ukizingatia kipindi hiki baadhi ya maeneo kuripotiwa kuwa na kipindupindu hata hivyo kwetu sisi hatujapata taarifa ya ugonjwa huo.
Ameongeza kuwa wananchi wanatakiwa kuendelea kutunza manzingira na kuchemsha maji ya kunywa pia kula chakula kilichoandaliwa vizuri pamoja hifadhi mazingira ya choo.
Aidha amesema wananchi wanatakiwa kuzingatia siku za usafi ambao kwa halmashauri alhamisi kila week inatumika kufanya usafi wa mazingira na jumamosi ya mwisho wa mwezi hivyo kutumia muda huo kufanya usafi kama inavyotakiwa.

# 04 WAZEE NA WATU WENYE ULEMAVUWA KASULU MJI WAPATIWA VIFAA WEZESHI




Wazee na watu wenye ulemavu wa Halmashauri ya Mji Kasulu wapatiwa vifaa wezeshi na shirika la HelpAge Tanzania kwa ajili ya kutengeneza zana wezeshi ikiwemo magongo na fimbo za kutembelea ili kupunguza changamoto zinazotokana na uzee na ulemavu .

Vifaa hivyo vimetolewa Januari 11 mwaka huu katika ukumbi wa chuo cha ualimu Kasulu mara baada ya kuwapatia mafunzo ya utengenezji vifaa tiba.

Akizungumza mara baada ya utoaji wa vifaa hivyo mteknolojia viungo tiba na vifaa tiba saidizi Florence Audax Greygory alisema lengo la kutoa vifaa hivyo ni kupunguza adha inayotokana na uzee na ulemavu hasa zinazohusiana na mjongeo.

“Tunaamini mtu anapozeeka utendaji wa mwili unapungua sio kama alipokua kijana hivyo anahitaji vifaa vya kumuwezesha kutembea lakini pia kwa mtu mwenye ulemavu anapata changamoto ya kutembea mwendo mrefu au kufanya shughuli za kila siku.”

Kwa upande wa afisa ustawi wa Halmashauri ya Mji Kasulu Festo Poncian Solly alisema mafunzo hayo yanatija na kimsingi vifaa hivyo ambavyo hutumika mara nyingi wanavipata kwa kuomba masaada au kununua kwa gharama kubwa.

hivyo wanapopata fura ya kujifunza na kupata vitendea kazi hii itawasaidia sana pia kwa upande wa maendeleo wanaweza kutumia elimu hio kutengeneza vifaa kwa ajili ya kuuza na kusaidia wengine

Akizungumza wakati wa kupokea vifaa hivyo, mwenyekiti wa wazee Kasulu amesema wanafurahi HelpAge kwa kuwapa vifaa hivyo kwa kuwawezesha kumudu kutengeneza vifaa vyao wenyewe.

“Tunayo furaha kuwezeshwa na manuufaa ya kujifunza kutengeneza fimbo za kutembelea na baadae tutaweka utaratibu kupitia ustawi wa jamii kuandaa mafunzo kwa kata nyengine ili kuweza kufikia watu wengi zaidi

Mradi huu umelenga kuwafikia wazee na watu wenye ulemavu Kigoma umeanzia katika Halmashauri ya Mji Kasulu na baadae kwenda kwenye maeneo mengine ndani ya mkoa wa Kigoma ukiwa na lengo la kupunguza adha zinazotokana uleamavu na uzee pia kuondoa changamoto ya upatikanaji wa vifaa saidizi ambavyo vina viwango ya vfaa tiba.

# 05 WADAU WA ELIMU HALMASHAURI YA MJI KASULU WASISITIZWA KUTOA ELIMU YENYE TIJA.







Mbunge wa Kasulu mjini Mh Joyce Ndalichako Amewataka walimu wa shule za msingi na sekondari wilayani Kasulu kutoa elimu yenye tija kwa wanafunzi. Hayo yamejiri katika kikao cha wadau wa elimu wilayani Kasulu kilichofanyika Januari 20 mwaka huu katika ukumbi wa Chuo cha ualimu Kasulu.

Akihutubia katika kongamano hilo waziri Ndalichako Amesema ni jukumu la walimu kuhakikisha wanasimamia elimu ili kuleta matokeo chanya kwa taifa la Tanzania.

"wanafunzi watoke wakiwa wameiva kwa kweli bila kufanya hivyo tutakua wahujumu uchumi maana tumeletewa hela nyingi tusiposimamia zitakua zimepotea wakati lengo lilikua ni kutengeneza msingi mizuri kwasababu serikali ya Dk Samia Suluhu Hassan inatambua kwamba elimu ndio msingi wa maendeleo yote. "

Aidha Amewataka wakuu wa shule kuwa wabunifu katika mbinu za kutoa chakula mashuleni wakishirikisha wazazi ili kuhakikisha wanafunzi wanapata chakula kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa kwa lengo la kutatua changamoto za upatikanaji wa chakula mashuleni. Ameyasema haya baada ya wakuu hao washule kuelezea namna wanavyopata changamoto katika kutoa chakula mashuleni ikiwemo watoto kutokurudi mchana wanapokwenda majumbani kwaajili ya chakula.

Akihitimisha kwenye kongamano hilo Mkuu wa Wilaya ya Kasulu Kanali Isack Mwakisu amewasisitiza walimu kupiga vita vitendo vinavyofaanywa na waganga wa jadi maarufu kama kamchape akidai vitendo hivyo hufitinisha serikali na wananchi wake na kwamba serikali haiwajatuma waganga hao kama wanavodai huku ikiendelea kuwachukulia hatua.



# 06 USIMAMIZI MZURI WA MIKOPO YA ASILIMIA KUMI MAPATO YA NDANI KUWANG'ARISHA VIONGOZI WILAYA NA HALMASHAURI.

Mwenyekiti wa Vijana CCM Taifa Mohammed Ali Kawaida ameipongeza Halmashauri ya Mji Kasulu kwa kuweza kusimamia miradi ya vijana iliyoanzishwa kwa fedha za mkopo wa asilimia 4 za Halmashauri kwa vijana

Ametoa pongezi hizo wakati akikagua mradi wa kikundi cha Vijana Iposa kalema wakati wa ziara yake wilayani kasulu iliofanyika januari 25 mwaka huu katika eneo la kiwanda cha vijana Iposa pamoja na kuwapongeza Vijana waliofaidika na fedha za mkopo huo huku akieleza zamira za mikop hiyo ni Kuwezsha Vijana kujiajiri na kujipatia kipato wenyewe.

Aidha Ameelezea lengo la Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Dokta Samia Suluhu Hassan kusitisha mikopo hiyo ni kufuatilia utekelezaji utaratibu mzuri kuhakikisha Vijana wanaostahili kupata mikopo hio wanaipata

"kwa bahati mbaya Kuna baadhi ya maeneo fedha zilikua zikitumika vibaya

Dk Samia akasema anasitisha mikopo ili kutekeleza utaratibu mzuri ili kuhakikisha Vijana wa

kimaskini waweze kunufaika na dhamira hiyo bado anayo na anaendelea nayo"

Awali akimkaribisha Mwenyekiti huyo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kasulu Dollar Rajab Kusenge Ameelezea namna ya uanzishwaji wa Mradi wa Vijana wa Iposa Kalema ambao wamefaidika kwa kupewa kiasi cha shilingi TShs 125 pamoja na eneo la kuanzisha Mradi huo

"kiwanda hiki wamejenga wenyewe kila kitu kuanzia msingi walianza kupewa elimu kupitia program ya Iposa nami niliwafanyia majaribio ya vitendo mpka walipoweza kufanya kazi tu kawapa pesa"

Kabla ya kusitishwa kwa mkopo wa vijana na Mh Dokta Samia Suluhu Hassan 4% ya mikopo ya halmashauri ilikua inatolewa kwa Vijana kwa lengo la kuwawezesha Kujikwamua kiuchumi na kupunguza changamoto ya upatikanaji wa ajira mchini.

# 07 MATUKIO YA PICHA KATIKA SHEREHE ZA UGAWAJI MICHE YA KAHAWA ILIYOANDALIWA NA TACRI KATA YA MSAMBARA



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kasulu Mh Noel.Hanura akikata utepe.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kasulu akiwa na mkuu wa Idara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi wakipokea miche ya kahawa. kwa ajili ya kupanda



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kasulu Noel Hanula akipanda mche wa kahawa katika shaba darasa



Mkuu wa idara ya kilimo ufugaji na uvuvi Dk Sudy M.Kundelya akipanda mche wa kahawa



Mkuu wa idara ya kilimo ufugaji na uvuvi Dk Sudy M.Kundelya akionja kahawa iliondaliwa na TACRI.

# MATUKIO YA PICHA YA ZIARA YA MWENYEKITI UMOJA WA VIJANA TAIFA ALIPOTEMBELEA MIRADI YA MAENDELEO KWAVIJANA KASULU MJI JAN 25 2024.



M/kiti wa UVCCM Taifa Mohammed Ali Kawaida (katikati) akielekea kukagua mradi wa vijana FAO Kidyama.



Mbunge wa jimbo la Kasulu mjini Prof. Joyce Lazaro Ndalichako akizungumza mbele ya mwenyekiti wa UVCCM Taifa mara baada ya ukaguzi wa mradi.



M/kiti wa UVCCM Taifa akipokea maelezo toka kwa kiongozi wa vijana wa FAO Kidyama namna wanavyoendesha shughuli ya ufugaji kuku.



Kijana toka kikundi cha FAO Kidyama akitoa maelezo namna mtambo wa kutotolea mayai (incubator) unavyofanya kazi.



Bidhaa ya bidhaa(mafuta ya nta pamoja na asali ya nyuki wadogoo na wakubwa) zinazotengenezwa na vijana hao.



M/kiti wa UVCCM Taifa Mohammed Ali Kawaida (katikati) akionja asali inayotokana na nyuki wadogo.



**LIMETOLEWA NA;**

**Kitengo Cha Mawasiliano Serikalini**

**Halimashauri ya Mji Kasulu**

kasulu_town_council | habari kasulu town council | www.kasulutc.go.tz

# JAN 2024

# Kasulu Yetu

Buzuka Design